https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kuumbwa kwa Ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo

https://www.path-2-happiness.com/sw

Yaliyomo

Kuumbwa kwa ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo

Je, umewahi kufikiria Umbile la Ulimwengu?!

Hekima ya kuumbwa kwaulimwengu

Kuumbwa na kukirimiwa kwamwanadamu

Mwanamke kukirimiwa sawa na mwanamume

Hekima ya kuumbwa kwa

mwanadamu

Baada ya hapo ewe mwanadamu…

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kuumbwa kwa Ulimwengu na Mwanadamu... Hekima, Kukirimiwa na Lengo

Ewe Mola Wangu!

"Nilipoona baadhi ya picha za anga za hivi karibuni jibu langu la kwanza lilikuwa ni kupiga mayowe nikisema Ewe Mola wangu! Kazi imezaa matunda. Kwa ujumla wake katika umri wangu hicho ni kitu cha kuvutia!!!"

Dr. Paul Murdin

Professor wa Mambo ya Unajimu Chuo Kikuu cha Cambridge

Je, umewahi kufikiria Umbile la Ulimwengu?!

Kwa hakika tafakuri ya Viumbe vya Allah ni moja ya njia nyingi ambazo zinampelekea mtu katika imani, huzidisha yakini kwa mwanadamu, na kumtambulisha kwa ukubwa wa Muumba na upeo wa elimu na hekima yake, Allah Ta'ala Ndie aliyeumba mbingu na ardhi kwa haki, hakuziumba kwa batili wala kwa mchezo wala hakuumba hivi hivi bila ya lengo. Allah Ta'ala amesema: {Mwenyezi Mungu ameumba mbingu na ardhi kwa Haki. Kwa hakika katika hayo ipo Ishara kwa Waumini.}[29:44].

Katika ulimwengu huu kuna viumbe kiasi gani ambao hawahesabiki! Unadhani wameumbwa kwa hekima ipi?!

Katika Ulimwengu huu kuna alama na dalili mbali mbali ambazo zinaonyesha kwa uwazi uwezo wa Allah Ta'ala na elimu mambo leo inaendelea kuvumbua na kutafiti dalili na alama mbali mbali ambazo zina mfanya mwanadamu ahisi utukufu wa Muumba huyu.

Lau mtu akifikiri kwa undani zaidi kwa Ulimwengu huu na yaliyomo katika Viumbe vya Allah atayakinisha ukamilifu wa yakini kuwa Ulimwengu huu

https://www.path-2-happiness.com/sw

umeumbwa kwa uwezo usio na ukomo kwa ufanisi wa hali ya juu kabisa, na aliyeumba ni Mungu Mwenye hekima, mwenye uwezo, Mjuzi amepima na akaufanyia uzuri kipimo chake.

Inatosha kufahamu kwa kuzingatia ya kuwa ndani ya Ulimwengu huu na mbingu zake na sayari na nyota zake na yaliyomo kama vile ardhi yetu, bahari, mito, ardhi, milima, wanyama, na miti ambayo imeumbwa na Allah na ambayo haikuwepo hapo kabla ili ipate hisia ni kiasi gani uwezo wa Allah, elimu yake na hekima yake, Allah Ta'ala amesema: {Je! Hao walio kufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi tukazibabandua? Na tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini? Na tukaweka katika ardhi milima iliyo thibiti ili isiwayumbishe, na tukaweka humo njia pana ili wapate kuongoka. Na tukaifanya mbingu kuwa dari iliyo hifadhiwa, lakini wanazipuuza Ishara zake. Na Yeye ndiye aliye umba usiku na mchana na jua na mwezi, vyote katika anga vinaogelea. } [21:30-33].

Na pindi mwenye akili anapofikiria katika viumbe wa Allah, mtu anakuwa anafahamu kwa elimu ya yakini kuwa yaliyo katika Ulimwengu huu yanamuabudu Mola wake; kila kiumbe chake kinamsabihi kwa himidi zake Allah, Allah Ta'ala amesema: {Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu, Mwenye hikima.}[62:1]

Na kusujudu kwa utukufu wake, Amesema Allah Ta'ala {Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18].

Vivyo hivyo, viumbe hivi vinamsabihi Allah Ta'ala na kumswalia, Allah amesema: {Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu vinamtakasa vilivyomo katika mbingu na ardhi, na ndege wakikunjua mbawa zao? Kila mmoja amekwisha jua Sala yake na namna ya kumtakasa kwake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kuyajua wayatendayo.}[24:41],

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hivyo basi muumini ataona kuwa Ulimwengu wote huenda na kutembea kama vile ni msafara mmoja katika muelekeo mmoja kwa Allah, hivyo basi pia atakwenda kwa furaha kwa muelekeo huu mzuri uliobarikiwa na maisha yake na utulivu wa roho yake.

Miongoni mwa dalili za Uungu

"Kuona kwangu sayari yetu ilikuwa ni ishara (maono) ya kiungu."

Edgar Mitchell

Wa sita katika wanaanga waliokwenda mwezini

Huu ni Uumbaji wa Mungu!!

"Kuona jambo hili kutambadilisha mwanadamu, na kumfanya mtu kuthamini viumbe vya Mungu na kumpenda Mungu." Akizungumzia kuhusu Ulimwengu.

James Irwin

Mwanaanga

Mungu Kumkirimu Mwanadamu.

Uislamu ambao ni kanuni ya Mwenyezi Mungu tunauona ukiwa ni wazi katika mazingira yanayotuzunguka; Kwa maamrisho pekee ya Mwenyezi Mungu, milima, bahari, sayari, nyota zinakwenda na kuongoka katika mapito yake (mzunguko wake). Vivyo hivyo kila atom katika ulimwengu huu (hata viumbe visivyokuwa hai) ila mwanadamu amevuliwa (anaondolewa) katika kanuni hii; kwani Mwenyezi Mungu amempa uhuru wa kuchagua; kwa hiyo anaweza kujisalimisha kwa amri ya Allah au akaweka kanuni zake mwenyewe na kwenda katika dini yake ambayo anairidhia, kwa masikitiko njia ya pili ina vizuizi vikubwa."

Deborah Potter

Mwanahabari wa Kimarekani

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hekima ya kuumbwa kwa ulimwengu

1. Dalili ya Kumpwekesha Allah Ta'ala.

Kwa hakika Ulimwengu huu mpana na yaliyomo ndani yake katika viumbe na miujiza ni ushahidi mkubwa wa utukufu wa uwezo wa Allah Ta'ala na ukamilifu wa maumbile yake na hii ni dalili ya kumpwekesha Allah Ta'ala, na kuwa hana Mola asiyekuwa yeye wala Mungu asiyekuwa Yeye, Allah Ta'ala amesema: {Na katika Ishara zake ni kuwa kakuumbeni kwa udongo. Kisha mmekuwa watu mlio tawanyika kote kote. Na katika Ishara zake ni kuwa amekuumbieni wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao. Naye amejaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri. Na katika Ishara zake ni kuumba mbingu na ardhi, na kutafautiana ndimi zenu na rangi zenu. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa wajuzi. Na katika Ishara zake ni kulala kwenu usiku na mchana, na kutafuta kwenu fadhila zake. Hakika katika haya bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao sikia. Na katika Ishara zake hukuonyesheni umeme kwa kukutieni khofu na tamaa. Na hukuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo huifufua ardhi baada ya kufa kwake. Hakika katika hayo zipo Ishara kwa watu wanao zingatia. Na katika Ishara zake ni kuwa mbingu na ardhi zimesimama kwa amri yake. Kisha atakapo kuiteni mwito mmoja tu, hapo mtatoka kwenye ardhi. Na vyake Yeye vilivyo mbinguni na katika ardhi. Vyote vinamt'ii Yeye.} [30:20-26]

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Katika aya nyingine amesema: {Sema: Alhamdu Lillahi! Kuhimidiwa ni kwa Mwenyezi Mungu! Na amani ishuke juu ya waja wake alio wateuwa. Je! Mwenyezi Mungu ni bora, au wale wanao washirikisha naye? AU NANI yule aliye ziumba mbingu na ardhi, na akakuteremshieni maji kutoka mbinguni, na kwa hayo tukaziotesha bustani zenye kupendeza? Nyinyi hamna uwezo wa kuiotesha miti yake. Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali hao ni watu walio potoka. Au nani yule aliye ifanya ardhi mahali pa kutua, na akajaalia ndani yake mito, na akaweka milima? Na akaweka baina ya bahari mbili kiziwizi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Bali wengi wao hawajui. Au nani yule anaye mjibu mwenye shida pale anapo mwomba, na akaiondoa dhiki, na akakufanyeni warithi wa ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ni machache mnayo yazingatia. Au nani yule anaye kuongoeni katika giza la bara na bahari, na akazipeleka pepo kuleta bishara kabla ya rehema zake? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Ametukuka Mwenyezi Mungu juu ya wanao washirikisha naye. Au nani anaye uanzisha uumbaji, kisha akaurejesha? Na nani anaye kuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Je! Yupo mungu pamoja na Mwenyezi Mungu? Sema: Leteni hoja zenu kama nyinyi ni wasema kweli.} [27:59-64].

https://www.path-2-happiness.com/sw

2. Ulimwengu kudhalilishwa kwa ajili ya Mwanadamu:

Mwenyezi Mungu amemuacha huru mwanadamu na kuabudu vitu; na hivyo kujaalia vyote vilivyomo katika ardhi hii vikiwa vimedhalilishwa kwa ajili ya mwanadamu kama ni fadhila na takrima kwake kutoka kwa Allah peke yake; kwa lengo la kufanikisha uimarishaji wa ardhi, ukhalifa, na zaidi ni kukamilisha utekelezaji wa ibada ndani yake, na kudhalilishwa hapa ina maana mbili: kudhalilishwa kwa ajili ya kumfahamu Allah, fadhila zake, ukarimu na utukufu wake. Na kudhalilishwa kwa maana ya kumkirimu mwanadamu na kunyanyua hadhi yake ukilinganisha na vile vilivyodhalilishwa kwake; Allah Ta'ala amesema: {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake….} [45:13]

Na amesema vile vile Allah mtukufu: {Mwenyezi Mungu ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi, na akateremsha maji kutoka mbinguni. Na kwa hayo akatoa matunda kuwa ni riziki yenu. Na akafanya yakutumikieni majahazi yanayo pita baharini kwa amri yake, na akaifanya mito ikutumikieni. Na akalifanya jua na mwezi kwa manufaa yenu daima dawamu, na akaufanya usiku na mchana kwa manufaa yenu. Na akakupeni kila mlicho muomba. Na mkihisabu neema za Mwenyezi Mungu hamwezi kuzidhibiti. Hakika mwanaadamu ni dhaalimu mkubwa, mwenye kuzikufuru neema.} [14:32-34]

Miongoni mwa dalili za Utume.

"Vipi Muhammad (mtu asiyesoma yaliyoandikwa) ambaye amekulia katika jamii ya Jaahiliya amejua miujiza ya Ulimwengu ambayo imeelezwa na Qur-aan Tukufu. Ambayo hadi hivi sasa sayansi inaendelea kuyatafiti?! Hapana shaka basi maneno haya kuwa ni maneno Mwenyezi Mungu Aliyetukuka.

Deborah Potter
Mwanahabari wa Kimarekani

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

3. Huenda Mkayakinisha kukutana na Mola wenu:

Hakika katika umbile la mbingu na ardhi (tuache suala la kuumbwa kwa mwanadamu) ni uthibitisho ulio wazi kuhusu ufufuo baada ya kifo, je, haikuwa suala la kurejesha maumbile ni rahisi na mepesi zaidi kuliko kuumba mara ya kwanza?! Allah Ta'ala amesema: {Na Yeye ndiye anaye anzisha uumbaji, kisha ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi kwake….}[30:27]

Bali kwa hakika kuumbwa mbingu na ardhi ni kukubwa kuliko maumbile ya mwanadamu, Allah Ta'ala amesema: {Bila ya shaka kuumba mbingu na ardhi ni kukubwa zaidi kuliko kuwaumba watu. Lakini watu wengi hawajui.} [39:57]

Na Allah Mtukufu akasema: {Mwenyezi Mungu aliye ziinua mbingu bila ya nguzo mnazo ziona, ametawala kwenye Ufalme wake, na amefanya jua na mwezi yamt'ii, kila kimoja kinakwenda kwa kiwango maalumu. Anayapanga mambo, na anazipambanua Ishara ili mpate kuwa na yakini kukutana na Mola wenu Mlezi.} [13:2].

Haki ni Moja

"Kuangalia aina hii ya kiumbe wala usimuamini Mwenyezi Mungu hilo kwangu mimi ni jambo lisilowezekana ….Hili limezidisha imani yangu. Natamani pawepo na maneno yenye kuelezea tukio hili.

John Glenn

Mwanaanga wa kwanza wa Kimarekani

Uko wapi ndani ya Ulimwengu huu.

"Picha hii ni ya mkusanyiko mkubwa wa sayari (galaxies) Sehemu yake ndogo huwakilisha sayari na njia zake ni zaidi ya 1,000,000,000,000 ya jua. Na jua ni kubwa kuliko ardhi kwa mara 1,300,000, na ardhi ni kubwa kuliko nyumba yako (kwa mfano ukubwa wa nyumba yako ni mita 500)kwa mara 1,020,144,000,000 na nyumba yako ni kubwa kuliko wewe mwenyewe kwa mara ngapi."?!'

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



Tone katika Bahari

"Hadi hivi sasa nyota kubwa iliyoumbuliwa ni VY Canis Majoris iko mbali nasi kwa masafa ya miaka elfu tano ya mwanga na ni kubwa kuliko jua kwa 9,261, 000,000 yaani 9 Bilioni na mara 261 milioni!! Na jua ni kubwa kuliko ardhi yetu kwa mara 1,300,000.

Kuumbwa na kukirimiwa kwa mwanadamu

Pamoja na utukufu wa umbile la mbingu na ardhi isipokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu amemdhalilishia hilo mwanadamu na kujaalia vitu hivyo kudhalilika kwake: Pamoja na utukufu wa umbile la mbingu na ardhi isipokuwa ni kwamba Mwenyezi Mungu amemdhalilishia hilo mwanadamu na kujaalia vitu hivyo kudhalilika kwake: {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake….} [45:13];

Na hilo ni kwa kumkirimu yeye mwanadamu na kumfadhilisha yeye kuliko viumbe vingine vyote, Allah Ta'ala amesema: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.} [17:70]

Allah amemuumba mwanadamu na kumjulisha kisa cha kuumbwa kwa Adam na kukirimiwa, kisha kumteremsha kutoka peponi kushuka ardhini kwa wasiwasi wa shetani na dhambi zake, kisha kutubia kwake, Allah amesema: {Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia Malaika: Msujudieni Adam. Basi wakasujudu isipo kuwa Iblisi, hakuwa miongoni mwa walio sujudu. Mwenyezi Mungu akasema: Nini kilicho kuzuia kumsujudia nilipo kuamrisha? Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, naye umemuumba kwa udongo. Akasema: Basi teremka kutoka humo! Haikufalii kufanya kiburi humo. Basi toka! Hakika wewe u miongoni mwa walio duni. Akasema: Nipe muhula mpaka siku watakapo fufuliwa. Akasema: Utakuwa miongoni mwa walio pewa muhula. Akasema: Kwa kuwa umenihukumia upotofu, basi nitawavizia katika Njia yako Iliyo Nyooka. Kisha

https://www.path-2-happiness.com/sw

nitawazukia mbele yao na nyuma yao na kuliani kwao na kushotoni kwao. Wala hutawakuta wengi wao wenye shukrani. Akasema: Toka humo, nawe umekwisha fedheheka, umekwisha fukuzwa. Hapana shaka atakaye kufuata miongoni mwao, basi nitaijaza Jahannam kwa nyinyi nyote. Na wewe, Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani hii, na kuleni humo mpendapo. Wala msiukaribie mti huu, mkawa katika wale walio dhulumu. Basi Shet'ani aliwatia wasiwasi ili kuwafichulia tupu zao walizo fichiwa, na akasema: Mola Mlezi wenu hakukukatazeni mti huu ila msije mkawa Malaika, au msije mkawa katika wanao ishi milele. Naye akawaapia: Kwa yakini mimi ni miongoni wa wanao kunasihini. Basi akawateka kwa khadaa. Walipo uonja ule mti, tupu zao zilifichuka na wakaingia kujibandika majani ya Bustanini. Mola wao Mlezi akawaita: Je, sikukukatazeni mti huo, na kukwambieni ya kwamba Shet'ani ni adui yenu wa dhaahiri? Wakasema: Mola wetu Mlezi! tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika. Akasema: Teremkeni! Mtakuwa nyinyi kwa nyinyi maadui. Na kwenye ardhi itakuwa ndio makao yenu na starehe yenu mpaka ufike muda. Akasema: Humo mtaishi, na humo mtakufa, na kutoka humo mtatolewa.} [7:11-25]

Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu sura nzuri kabisa, kisha akampulizia roho yake, hivyo mwanadamu akatokea katika umbile zuri kabisa anasikia na kuona na kutembea na kuzungumza: {…Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.} [23:14]

Na akamfundisha kila anachohitaji kukifahamu na akampa sifa na vipawa ambavyo hakumpa kiumbe mwingine kama vile: Akili, Elimu, ubainifu, kuongea, umbile, sura nzuri, umbile lililokirimiwa na kiwiliwili cha kati na kati, na kuweza kupokea elimu mbalimbali na kutumia dalili kwa fikra na kuongoza katika tabia njema na sifa nzuri kabisa na akamkirimu na kumfadhilisha kuliko viumbe vingi; katika mandhari ya kukirimiwa hivi kwa mwanadamu iwe kwa mwanamume au mwanamke.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Binadamu wote ni sawa.

"Watu wote huzaliwa huru wakiwa sawa katika utukufu na haki, na wamepewa akili na dhamira. Na ni juu yao kuamiliana baadhi yao kwa wengine kwa roho ya udugu.

Mada ya kwanza katika tangazo la kimataifa la haki za binadamu.

-Hakika Allah amemuumba mwanadamu kwa mkono wake tokea kuumbwa kwake wakati wa kuumbwa kwa Adam ('Alayhi Salaam); na huu ni utukufu na kukirimiwa hakuna utukufu zaidi ya huu; Allah Ta'ala amesema:

{Mwenyezi Mungu akamwambia: Ewe Iblisi! Kipi kilicho kuzuia kumt'ii yule niliye muumba kwa mikono yangu? Je! Umejiona mkubwa, au umekuwa katika wakuu kweli?} [38:75]

-Hakika Allah Ta'ala amemuumba mwanadamu katika umbile zuri; Allah amesema, {Bila ya shaka tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.} [95:4]

Na akasema vile vile: {…na akakupeni sura, na akazifanya nzuri sura zenu. Na marudio ni kwake} [64:3].

-Mwenyezi Mungu Mtukufu amemkirimu mwanadamu huyu wa kuamrisha Malaika wake kumsujudia Adam, Baba wa wanadamu, aliposema Allah Ta'ala: {Na pale tulipo waambia Malaika: Msujudieni Adam. Wakamsujudia isipo kuwa Iblisi….} [17:61].

-Allah Ta'ala amemkirimu mwanadamu huyu na akamneemesha kwa akili, kufikiria, kusikia, kuona na hisia nyingine za fahamu, Allah Ta'ala amesema: {Na Mwenyezi Mungu amekutoeni matumboni mwa mama zenu, hali ya kuwa hamjui kitu, na amekujaalieni masikio na macho na nyoyo ili mpate kushukuru.} [16:78].

-Allah Ta'ala alimpulizia roho; na hapo ndipo daraja lake likawa la juu, Allah akasema: {Na nitakapo mkamilisha na kumpulizia roho inayo tokana nami, basi muangukieni kwa kumt'ii.} [38:72]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na huu ni ukarimu mkubwa alioupata mwanadamu; na ndipo ilipopasa mwanadamu kuheshimiwa kama mwanadamu, sasa iweje mwanadamu huyu amfanyie uadui yule aliyempulizia roho Allah Ta'ala.?!!

Allah Ta'ala akamfanya kuwa ni Khalifa katika ardhi, na sio Malaika au Jini; Allah akasema: {Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua.} [2:30]

Na huu ni utukufu mkubwa ambao Malaika hawakuupata ambao hawamuasi Allah alichowaamuru, na ambao daima wapo katika kumdhukuru, kumtakasa na kumtukuza Allah Ta'ala.

Ujumbe wetu

"Allah ametutuma kuwatoa watokao kwenye kuabudu watu kuelekea kwenye kumuabudu Allah. Na kutoka katika mashaka ya dunia kuelekea kwenye upana wake, na kutoka kwenye dhuluma ya dini kwenda kwenye uadilifu wa Uislamu"

Ribi'I bin 'Amir

Miongoni mwa sahaba wa Mtume (Swalla Llahu 'alayhi wasallam)

-Allah Ta'ala amemdhalilishia mwanadamu huyu yote yaliyomo hapa ulimwenguni kwa mbingu zake na ardhi yake, na yaliyomo baina yake na ndani yake katika jua, mwezi, nyota na sayari. Allah Ta'ala amesema: {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri. } [45:13],

-Kuwa Allah Ta'ala amemkomboa mwanadamu na amemuacha huru na utumwa wowote kwa kiumbe chochote (kingine) kadiri ya ubora wake au ukubwa wake, na hicho ni kilele cha uhuru aliokuwa nao mwanadamu; kwa jinsi alivyohamishwa kutoka katika kunyenyekea kwa mwanadamu na kumuabudu mwanadamu mwenzake hadi kumuabudu Allah Ta'ala, na kuabudu huku kwa ajili ya Allah ndio kilele cha uhuru dhidi ya kumuabudu asiyekuwa Yeye. Na hii ndio maana Allah akakataa kuwepo kwa wakala baina yake na waja wake; kwani kuna baadhi ya watu wamejiwekea na kuzusha wakala baina ya mwanadamu na Mola wake na wengine kwa hilo wamepewa

https://www.path-2-happiness.com/sw

sifa ya Uungu. Allah amemkirimu mwanadamu kwa sababu hakuna wakala baina yake na Mola wake, Allah amesema: {Wamewafanya makuhani wao na wamonaki wao kuwa ni marabi badala ya Mwenyezi Mungu, na pia Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa isipo kuwa wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo.} [9:31].

-Kumkomboa mwanadamu kutokana na khofu ya mustakbali na kukata tamaa, nayo ni kwa kupitia kuamini kwa hukumu (majaliwa) na kudura pamoja na kufuata sababu zote za kimaisha za kimaada; hivyo basi imani ya majaliwa na kudura ndio inayomfanya mwanadamu muumini katika hali ya usalama na amani, na katika hali ya utukufu na hisia ya karama na kuondokana na kero na huzuni au masikitiko yaliyopita madamu hakufanya mapungufu katika kuchukua na kutumia sababu mbali mbali. Kwa sababu yote ni kutoka kwa Allah, Allah Ta'ala amesema¨ {Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi.} [57:22],

Imani hii inamfanya mwanadamu kuwa katika mizani nzuri ya nafsi na utulivu mkubwa wa kweli; ambapo misiba haimuathiri wala haimfanyi kuwa muoga au mwenye huzuni kama ambavyo neema mbalimbali na furaha haimfanyi kuwa ni jeuri, mwenye kujiona na kujivuna

-Akili ya mwanadamu kuheshimiwa; Allah Ta'ala ameipa thamani kubwa sana akili ya mwanadamu pamoja na fikra zake Ameamuru kuangalia na kuchukua mazingatio, na kajaalia swala la kufikiria kuhusu kuumbwa kwa mbingu na ardhi na kusimamisha hoja na dalili mbali mbali kuwa ni faradhi; Allah Ta'ala amesema: {Sema: Angalieni yaliomo mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasio amini.} [10:101]

Hakuna mtu wa Kati

"Kuna jambo muhimu: Nalo kutokuwepo mtu wa kati baina ya mja na Mola wake. Na hili ndilo walilolipata wenye akili za kitendaji."

Etienne Denier

Mchoraji na Mwanafikra wa Kifaransa

Kadhalika Allah ameamuru akili ya mwanadamu iheshimiwe, kutunzwa, kuangaliwa vizuri, kuifanyisha kazi, kuishughulisha, na kutoyagandisha kwa njia ya kufuata mambo kibubusa na kutumia kasumba tu; Hakuna kukalifishwi ila kwa kutumia akili, kama vile ambavyo Mwenyezi Mungu alivyofanya akili ya mwanadamu kuwa ndio dalili ya kuwepo kwake Yeye Allah na hoja ya upweke wake; bali Allah amewataka wanadamu warejee kwenye akili pale wanapotofautiana; Allah Ta'ala amesema: {…Sema: Leteni ushahidi wenu kama nyinyi ni wasema kweli} [2:111]

Na akaikomboa akili kutokana na kila aina ya upotofu, ushirikina, udajali na kutegemea majini na mfano wa hayo.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

-Kuhakikisha na kuthibitisha kuwa kila mwanadamu ana majukumu (wajibu) na atahesabiwa kwa matendo yake, wala hakuna uhusiano wowote na matendo ya mtu mwingine, Allah Ta'ala amesema: {Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine…} [35:18]

Na kukirimiwa huku kwa mwanadamu ndani ya Qur-aan; kunafuta ile fikra ya dhambi ya asili, na kumkomboa na kumsafisha mwanadamu kutokana na mazito yake.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Mwanamke kukirimiwa sawa na mwanamume

Kukirimiwa mwanadamu hakukuishia tu kwa mwanamume bila ya mwanamke, au kwa jinsia moja bila ya nyingine, asili ya mwanamke ni sawa na ya mwanamume katika kukirimiwa na kutukuzwa sawa kwa sawa: {…Nao wanawake wanayo haki kwa Sharia kama ile haki iliyo juu yao….} [2:228]

Allah Mtukufu akasema: {Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi….} [9:71],

Wala mwanamke hatofautiani kabisa na mwanamume katika suala la malipo ya akhera, Allah amesema: {Mola Mlezi wao, akayakubali maombi yao akajibu: Hakika sipotezi kazi ya mfanya kazi miongoni mwenu, akiwa mwanamume au mwanamke, kwani ni nyinyi kwa nyinyi….} [3:195],

Na katika aya nyingine, Allah kasema: {Na anaye fanya mema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini - basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa hata kadiri ya tundu ya kokwa ya tende.} [4:124]

Allah amemkirimu mwanamke kama mwanadamu pindi alipo mzingatia kuwa ni mwenye kukalifishwa mwenye majukumu

Sawa kwa Sawa

"Chuo kikuu cha Oxford hakijatoa haki sawa baina ya wanafunzi wa kike na wa kiume (katika Michezo na Umoja wa wanafunzi); isipokuwa kwa uamuzi uliotolewa tarehe 21 Julai mwaka 1964."

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Muujiza ya kweli

"Ikiwa sisi tutalinganisha misingi ya Qur'ani na misingi ya jamii zote zilizopita; basi tutakuta kuwa Qur-aan ndio itakayokuwa imerikodi maendeleo ndani yake yasiokuwa na ubishi, na haswa haswa kwa munasaba wa Athens na Roma; ambapo mwanamke alikuwa na mapungufu kwa sura thabiti."

Roger Garoudye
Mwanafalsafa wa Kifaransa

kamili kama alivyo mwanaume na ni mwenye kulipwa thawabu na kuadhibiwa kama alivyo mwanaume, hata jukumu la mwanzo kabisa ambalo Mwenyezi Mungu amempa mwanadamu lilikuwa la wote kwa pamoja; yaani mwanamke na mwanaume; pale Allah alipowaambia wanadamu wa mwanzo ambao ni Adamu na mke wake: {Na tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani, na kuleni humo maridhawa popote mpendapo, lakini msiukaribie mti huu tu; mkawa katika wale walio dhulumu.} [2:35]

Kama ambavyo Allah hakumbebesha mzigo mwanamke kuwa ndiye aliyekuwa sababu ya kumtoa Adam peponi na tabu walizokuwa wakipata au kuendelea kuzipata vizazi vyao baada yao kama ilivyo katika dini nyinginezo, bali Allah amemtaja Adam kuwa ndie mhusika mkuu: {Na hapo zamani tuliagana na Adam, lakini alisahau, wala hatukuona kwake azma kubwa.} [20:115] {Basi wakaula wote wawili, na uchi wao ukawadhihirikia na wakaanza kujibandika majani ya Bustani. Na Adam akamuasi Mola wake Mlezi, na akapotea njia. Kisha Mola wake Mlezi akamteuwa, naye akamkubalia toba yake, naye akamwongoa. } [20:121-122].

Mwanamke katika Sheria za mwanadamu

"Huko Roma kulikuwa na mkutano mkubwa, ukitafiti mambo ya mwanamke. Maamuzi yakatolewa kuwa mwanamke hana roho (nafsi) na kwa sababu ya dosari hii hatarithi maisha ya akhera. Kadhalika mwanamke ni uchafu hapaswi kula nyama, wala kucheka, bali hata kuzungumza, na muda wake wote autumie katika swala, ibada na utumishi. Wakamkataza kufanya yote hayo wakamwekea kufuli la chuma mdomoni mwake; ikawa mwanamke katika familia za juu na za chini anatembea njiani na akienda na kurudi nyumbani kwake na huku mdomoni mwake kukiwa na kufuli. Hii ni mbali na mateso mengine ya kiwiliwili ayapatayo mwanamke huyu kwa kumzingatia kuwa yeye ni nyenzo ya upotoshaji anayotumia shetani kuharibu nyoyo."

Mwanamke mbele yao

Katika sheria za kale za Kihindi tunasoma: Maradhi, mauti, moto, sumu, nyoka na moto vyote hivyo ni bora kuliko mwanamke. Haki ya mwanamke ya kuishi huisha kwa kuisha haki ya mumewe ambae ndie bwana na mmiliki wake. Akiona maiti yake inaungua nae hujitupa kwenye moto ule, vinginevyo ni haki yake kupata laana ya milele.

Hivyo basi katika utu na ubinadamu ni kuwa mwanaume analingana na mwanamke sawa kwa sawa, Allah Ta'ala amesema: {Enyi watu! Hakika Sisi tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa ni mataifa na makabila ili mjuane. Hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni huyo aliye mchamngu zaidi katika nyinyi. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye khabari. } [49:13]

Hivyo ni kuwa mwanaume anashirikiana na mwanamke na wanafanana au wako sawa kwa sawa katika mambo yafuatayo:-

-Maendeleo ya mtu katika haki maalum za kumiliki: Haiba ya mwanamke ni yenye hadhi na kuheshimiwa kisheria, Allah amempa haki sawa na mwanaume katika Majukumu na utekelezaji wake, amemthibitishia haki yake ya kutumia na kuingia katika mkataba yote; kama haki ya kuuza, haki ya kununua na mfano wake, na haki zote hizi ni za wajibu kutekeleza bila ya kifungo chochote au kizuizi ambacho kitazuia uhuru wake wa kutekeleza, ila vizuizi vile ambavyo vina mzuia mwanaume vile vile, Allah Tabaaraka amesema: {…Wanaume wana fungu katika walio vichuma, na wanawake wana fungu katika walio vichuma…} [4:32],

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kadhalika amempa haki ya kurithi, Allah Ta'ala amesema: {Wanaume wana sehemu katika wanayo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Na wanawake wanayo sehemu katika waliyo yaacha wazazi na jamaa walio karibia. Ikiwa kidogo au kingi. Hizi ni sehemu zilizo faridhiwa.} [4:7]

Na akamfanya mwanamke mbele ya sheria sawa na mwanaume anapopatia au kukosea; Allah amesema: {Na mwizi mwanamume na mwizi mwanamke, ikateni mikono yao, hayo ni malipo ya waliyo yachuma, ndiyo adhabu ya mfano itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima.} [5:38].

-Malipo ya Akhera; Allah amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97]

Urafiki na kunusuriana. Allah amesema: {Na Waumini wanaume na Waumini wanawake wao kwa wao ni marafiki walinzi. Huamrisha mema na hukataza maovu, na hushika Sala, na hutoa Zaka, na humt'ii Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} [9:72].

Ni Jeuri gani hii?!!!

"Mwanamke kwa mwanamume ni kama mtumwa kwa bwana wake. Au ni kama vile kazi za mikono ukilinganisha na kazi za akili. Au ni kama mfano wa Mshenzi na Myunani. Mwanamke ni mwanamume mpungufu, ameachwa amesimama katika daraja la chini kwenye ngazi ya maendeleo."

Aristotle

Mwanafalsa wa Kigiriki

Mwanamke wa Kifaransa

"Huko Ufaransa moja katika majimbo yake kulifanyika mkutano mwaka 586 mazungumzo yalihusu mwanamke: Je, ni mwanadamu au sio mwanadamu? Hitimisho lilikuwa ni uamuzi wa waliohudhuria kuwa mwanamke ni binadamu, lakini ameumbwa kumuhudumia mwanamume, katika mwezi wa Februari mwaka 1938 ilitolewa kanuni ya kufuta kanuni zingine zilizokuwa zikimkataza mwanamke wa Kifaransa katika baadhi ya matumizi ya mali (baada ya hapo kuruhusu) na kwa mara ya kwanza katika historia ya mwanamke wa Kifaransa aweze kufungua akaunti kwa jina lake katika mabenki.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Haki za Mwanamke Zimemezwa

"Nikageuka, na moyo wangu ulikazwa katika kujua na kupeleleza, na kuitafuta hekima, na maana ya mambo yaliyoko; ili nifahamu ya kuwa uovu ni upumbavu, na upumbavu ni wazimu. Nami nimeona lililo na uchungu kupita mauti; yaani, mwanamke ambaye moyo wake ni mitego na tanzi, na mikono yake ni kama vifungo." (Mhubiri 7:26

Kitabu Kitakatifu- Agano la kale

Sawa kwa Sawa

"Katika kivuli cha Uislamu mwanamke amerejesha uhuru wake, na akapata hadhi ya juu: Uislamu unawazingatia wanawake kuwa ni ndugu walio sawa na wanaume, na kila mmoja anamkamilisha mwingine, Uislamu umelingania taaluma ya mwanamke na kumzawadia elimu na utamaduni. Kwa hiyo ukampa haki ya kumiliki na uhuru wa kutumia anachomiliki, kama ambavyo umempa haki ya kuvunja mkataba wa ndoa na uhuru wa kufikiri na kujieleza."

Mona Cluskey

Mwanadiplomasia wa Kijerumani

«Yamekuja maamrisho ya kumhurumia mwanamke na kumfanyia wema; Allah ameharamisha wanawake kuuwawa katika vita, na akaamrisha kukaa pamoja na wanawake wenye hedhi na kufanyia nao uwakala na wakati huo Mayahudi walikuwa wanakataa hilo na kuwatenga na kuwadharau wala hawafanyi nao uwakala hadi watoharike, mwanamke katika zama za Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) walikirimiwa kwa hali ya juu pindi aliposema: "Mbora wenu ni mbora wenu katika familia yake, na mimi ni mbora wenu kwa familia yangu.» (Imepokewa na Tirmidhi, na akasema hadithi hii ni Hassan Sahihi).

«Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alikasirika pale mwanamke alipopigwa katika zama zake, na kusema: "Mmoja wenu anampiga mke wake kipigo cha mtumwa, kisha jioni humkumbatia» (Al-Bukhari).

«Na wakati kundi la wanawake lilipokuja kuwashitaki waume zao kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam); Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alisema: "Wanawake wengi wamekuja katika nyumba ya Muhammad kuwashitakia waume zao, wao (waume) hawakuwa bora kwao.» (Abu Dawuud).

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Mwanamke amepewa ambayo hajapewa mwanaume; Allah ameamrisha mama afanyiwe wema zaidi kuliko baba wakati mmoja mtu mmoja alikuja kwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: «Ewe Mtume wa Allah ni nani mwenye haki ya kusuhubiana nae –katika riwaya nyingine wema –Mtume akasema: Mama yako, akauliza: Kisha nani? Akasema: Mama yako, akauliza: Kisha nani? Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: Baba yako.» (Al-Bukhari na Muslim).

Na hivyo Mtume kuyafanya malezi ya watoto wa kike yana ujira mkubwa kuliko malezi ya watoto wa kiume; Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Atakayejaribiwa (kuwa) na wasichana hawa kisha akawafanyia wema, watakuwa sitara yake na moto» (Bukhari na Muslim)

Na akaseme tena Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam):

«Ewe Mola kwa hakika mimi nasikitishwa (kwa kutotolewa) haki za wanyonge wawili; yatima na mwanamke» (Hadithi Hassan, imepokewa na An-Nasai kwa sanad nzuri)

Sheria za Mwanadamu zinadhulumu na ni jeuri

"Mfalme Henry wa nane alitoa kanuni ya kuharamisha mwanamke kusoma kitabu kitakatifu. Kama ambavyo mwanamke alikuwa akihesabiwa katika Sheria za jumla za Kiingereza katika mwaka 1850 kuwa si katika raia wake wala hawakuwa na haki zao binafsi, wala hata haki ya kumiliki nguo zao wala katika mali zao walizopata kwa jasho lao."

Mfalme Henry wa Nane

https://www.path-2-happiness.com/sw

HEKIMA YA KUUMBWA KWA MWANADAMU

Mwanadamu huyu ambaye Allah amemdhalilishia kila kitu katika Ulimwengu huu na kumkirimu yeye peke yake na kuwaacha viumbe wengine, Allah amemuumba kwa hekima kubwa sana; Allah ameepukana na mchezo na ubatili, Allah amesema: {Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na kukhitalifiana usiku na mchana ziko Ishara kwa wenye akili, Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto.} [190-191]

Kadhalika Allah amezungumzia kuhusu dhana potofu ya makafiri: {Na hatukuziumba mbingu na ardhi na viliomo ndani yao bure. Hiyo ni dhana ya walio kufuru. Ole wao walio kufuru kwa Moto utao wapata.} [38:27]

Allah hakumuumba mwanadamu kwa ajili ya kula, kunywa na kuzaa tu, na kwa mfano huo wawe sawa na wanyama, bali Allah Ta'ala amemkirimu na kumfadhilisha mwanadamu kuliko wengi aliowaumba lakini watu wengi wamekataa na wamekufuru; hivyo wakajifanya hawajui au kukataa hekima ya kweli ya kuumbwa kwao, hamu yao kubwa ikawa ni kustarehe kwa matamanio ya kidunia, na maisha ya watu hawa ni kama vile maisha ya wanyama, bali duni zaidi kuliko wanyama, Allah Ta'ala amesema: {…Na walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.} [47:12]

Katika aya zingine Allah amesema: {Waache wale, na wastarehe, na iwazuge tamaa. Watakuja jua.} [15:3]

Kwa Mungu

"Kwa hakika dini na sayansi hupigana katika vita moja dhidi ya shaka, kupinga (dini) na uzushi na sauti yao moja katika vita hivi ni daima itakuwa: Tuelekee kwa Mwenyezi Mungu."

Marx Planck

Mwanzilishi wa nadharia ya Kwanta (Quantum)

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na: {Na tumeiumbia Jahannamu majini wengi na watu. Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walio ghafilika.} [7:179].

Watu wote wanalazimika kuamini kuwa viungo vyao vimeumbwa kwa hekima, huu ni uoni wa mazingatio kwa mfano masikio kwa ajili ya kusikilizia, na kadhalika…Je, inawezekana sasa viungo vya mwanadamu vikaumbwa kwa hekima halafu mwanadamu mwenyewe akaumbwa bila maana? Au ni kuwa haridhiki kumuitikia Mola wake ambaye amemuumba alipomjulisha hekima ya kuumbwa kwake?!

Hivyo basi ni kwa nini Allah ametuumba? Na kwa nini alitukirimu na kutudhalilishia kila kitu? Ametujulisha hilo Subhaanahu; Allah amesema: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. } [51:56],

Na Allah Mtukufu akasema vile vile: {AMETUKUKA ambaye mkononi mwake umo Ufalme wote; na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha.} [67: 1-2],

Na kinachofahamika kwa watu wenye akili ni kuwa mwenye kutengeneza kitu ndiye mwenye uwezo wa kukielezea hekima yake kuliko mtu mwingine, na kwa Mwenyezi Mungu kuna mifano mikubwa, kwani yeye ndiye aliyemuumba mwanadamu, naye anajua zaidi hekima ya kuumbwa kwake. Ibada hapa ufahamu wake ni mpana mno, mkubwa kuliko Swala, Funga, bali inaingia ndani yake

Hoja yenye nguvu

"Ni vigumu kwa mwanadamu kuleta taswira ya mwanzo wa uhai au kuendelea kwake bila ya kuwepo nguvu yenye kuumba yenye kutawala. Na mimi ninaamini kuwa Wanafalsafa katika tafiti zao za kifalsafa kuhusu maisha wamefumbia macho hoja yenye nguvu kuhusiana na mambo yalio katika Nidhamu (utaratibu) wa ulimwengu huu

Magnus Maclees

Mwanachama wa Chama cha Wanasayansi Uingereza

https://www.path-2-happiness.com/sw

kuimarisha ardhi yote, Allah Ta'ala anasema: {…Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu kwake. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi.} [12:61]

Na maisha yote ya mwanadamu ni ibada kwake Allah amesema: {Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote. Hana mshirika wake. Na hayo ndiyo niliyo amrishwa, na mimi ni wa kwanza wa Waislamu.} [6:162-163].

Ibada ni ufahamu mpana

Amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) «Ikisimama kiama na katika mkono wa mmoja wenu kuna mche basi na aoteshe.» (Ahmad). Wakauliza: Ewe Mtume wa Allah Je, mmoja wetu atayaendea matamanio yake kisha atakuwa na ujira? Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) akasema: «Je unaonaje kama angeyaweka katika haramu, Je atapata madhambi? Vivyo hivyo akiweka katika halali atapata nayo ujira.» (Muslim).

Hadithi tukufu

BAADA YA HAPO EWE MWANADAMU...

Ikiwa Ulimwengu huu wote umedhalilishwa kwa ajili yako na dalili mbali mbali, alama zake na ushahidi mbele ya macho yako zenye kushuhudia kuwa: Hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Allah Peke Yake hana mshirika, na pindi ujuapo Ewe mwanadamu ya kuwa ufufuo kwako na maisha yako na kufufuliwa baada ya kufa kwako ni jepesi mno kuliko kuumbwa kwa mbingu na ardhi, na ya kuwa Allah Ta'ala amekuumba kwa umbo lililo bora, na akakukirimu kwa takrima kubwa, na akakudhalishia Ulimwengu wote kwa ajili yako, sasa ni nini kikudanganyacho na Mola wako Mtukufu (hata ukamuasi)?! Allah amesema: {Ewe Mwanaadamu! Ni nini kikudanganacho na Mola wako Mtukufu Aliyekuumba.} [82:6-8]

Mwishowe wewe ni mwenye kukutana na Mola wako, Allah amesema: {Ewe mtu! Hakika wewe unajikusuru kwa juhudi kumwendea Mola wako Mlezi, basi utamkuta. Ama atakaye pewa daftari lake kwa mkono wa kulia, Basi huyo atahisabiwa hisabu nyepesi, Na arudi kwa ahali zake na furaha. Na ama atakaye pewa daftari lake kwa nyuma ya mgongo wake, Basi huyo ataomba kuteketea. Na ataingia Motoni. } [84:6-12]

Nenda katika njia ya furaha ya duniani na Akhera kwa maisha kwa lengo na hekima ya kuumbwa kwako, na hapo ndipo utakapopata furaha kwa ajili ya maisha yako, na utapata utulivu na kufurahia kukutana na Mola wako baada ya kifo chako.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Ulimwengu wote upo katika kumuabudu Mola wake, viumbe wake wote wanamsabihi na kumhimidi Mola wao, Allah Ta'ala amesema: {…Viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi vinamtakasa Mwenyezi Mungu…} [62:1]

Na vinasujudu kwa ukubwa wake: {Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18].

Bali viumbe vyote hivi vinaswali kwa ajili ya Mola wake kwa swala inayonasibiana nao, Allah amesema: {Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu vinamtakasa vilivyomo katika mbingu na ardhi, na ndege wakikunjua mbawa zao? Kila mmoja amekwisha jua Sala yake na namna ya kumtakasa kwake…} [24:41],

Je, inakulaiki wewe kukosa kuhudhuria katika tukio hili lenye kutisha? Baada ya hapo utakuwa ni mwenye kufedheheshwa; amesema kweli Allah Ta'ala: {Je! Huoni kwamba vinamsujudia Mwenyezi Mungu viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anaye fedheheshwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumhishimu. Hakika Mwenyezi Mungu hutenda apendayo.} [22:18]

https://www.path-2-happiness.com/sw

Je, hawazingatii?!

"Mimi nashangazwa kwa anayeangalia mbinguni na kuona ukubwa wa Uumbaji kisha asimuamini Mungu."

Abraham Linkolin

Raisi wa 16 wa Marekani.